TANGAZO LA SERIKALI NA. 699 la tarehe 02/12/ 2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA IGANDU, CHIBWE NA CHIMWAGA YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Igandu, Chibwe na Chimwaga ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba MV40 yenye majira - nukta 182724.4E, 9302220.69N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa $119.9^0$ kwa umbali wa kilomita 7.686 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MV61 yenye majira-nukta 189387.05E, 9298388.68N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa kufuata mipaka ya Wilaya na kukatisha Reli ya Kati katika uelekeo wa $188.03^0$ kwa umbali wa kilomita 7.811 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MV57 yenye majira - nukta 188296.15E, 9290654.65N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $308.298^0$ kwa umbali wa kilomita 4.14 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MV58 yenye majira - nukta 185047.04E, 9293220.42N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa $254.87^0$kwa umbali wa kilomita 3.24 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MV59 yenye majira - nukta 181916.96E, 9292374.13N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa $320.67^0$ kwa umbali wa kilomita 3.89 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MV43 yenye majira - nukta 179454.02E, 9295379.62N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo

*Tangazo la Serikali na. 698 (linaendelea)*

wa 346.84$^0$ kwa umbali wa kilomita 1.95 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MV42 yenye majira - nukta 179009.72E, 9297279.87N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa 340.71$^0$ kwa umbali wa kilomita 2.03 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MV41 yenye majira - nukta 178339.73E, 9299194.61N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa 45.54$^0$ kwa umbali wa kilomita 1.53 hadi alama ya mpaka ya upimaji namba MV39 iliyopo katika Reli ya Kati yenye majira - nukta 179433.16E, 9300267.79N; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa 59.32$^0$ kwa umbali wa kilomita 3.827 hadi ulipoanzia."

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*